(1)**Digrii ya heshima**: Hii hutolewa kwa ajili ya kutambua kazi na mchango mkubwa ulio tukuka ambao mtunukiwa kautoa kwa jamii husika. Mfano, Rais Mstaafu Jakaya Mrisho Kikwete alitunukiwa digrii za heshima kutoka vyuo vikuu zaidi ya 14 mbali mbali duniani (Kenya, Marekani, Ulaya, Asia, nk), ikiwemo na chuo kikuu chetu cha Nelson Mandela.

(2)**Shahada ya uzamivu** (doctorate degree) hii hujulikana kama digrii ya udaktari wa falsafa (PhD, japo yapo na majina mengine). Shahada hii hutolewa kwa walioisomea wakafanya tafiti za hali ya juu na kuandika tasnifu (thesis au dissertation) na machapisho mengine. Mfano, Rais wetu wa sasa, Mh. Dr. John Pombe Magufuli, anayo shahada hii ya uzamivu katika fani ya Kemia. Lakini pia katunukiwa digrii ya heshima na UDOM.

(3)**Shahada ya umahiri** (Master's degree) hii ni shahada ya pili

(4) **Shahada ya awali** au ya kwanza (bachelor's degree)

Wahitimu wetu tarajali:

Kwa kuhitimsha, kupitia mahafali haya, hadhara hii inawatuma muenende kwenye jamii ya Tanzania na Afrika kwa busara kuu na uadilifu uliotukuka kama ilivyoashiria kwenye mavazi yenu, na maandamano ya maprofesa na wahadhiri wenu. Umma huu unawapongeza sana na kuwatuma mkatumie elimu yenu, ubunifu wenu na busara zenu kuwa chachu ya kuleta maendeleo endelevu kwenye mataifa yenu na bara zima.

HONGERENI SANA!

THE NELSON MANDELA AFRICAN INSTITUTION OF SCIENCE AND TECHNOLOGY

HOTUBA YA MLAU WA TAASISI, PROFESA VERDIANA-GRACE MASANJA, KWENYE MAHAFALI YA SITA YA TAASISI YA SAYANSI NA TEKNOLOJIA YA NELSON MANDELA, ARUSHA-TANZANIA

29 Agosti 2020

Mkuu wa Taasisi ya Sayansi na Teknolojia ya Nelson Mandela (NM-AIST) na Makamu wa Rais Mstaafu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mhe. Dkt. Mohamed Gharib Bilal;

Mkuu wa Mkoa wa Arusha, Mh. Iddi Hassan Kimanta;

Mkuu wa Wilaya ya Arumeru, Mh. Jerry Muro;

Mwenyekiti wa Baraza la washauri la NM-AIST, Prof. Joseph Rwegasila Buchweishaija;

Makamu Mkuu wa NM-AIST, Prof. Emmanuel Joachim Luoga;

Wahitimu tarajali;

Makamu wakuu, Wakurugenzi na Viongozi wote wa Taasisi za Elimu ya Juu mliopo hapa leo;

Wakurugenzi wa Taasisi za Umma na Binafsi mliopo hapa;

Wajumbe wa Baraza la washauri la NM-AIST, Senate na Bodi ya Wadhamini;

Viongozi wa Dini;

Maofisa wa Serikali;

Wafanyakazi wote na wanafunzi wa NM-AIST;

Waandishi wa Habari;

Wageni Waalikwa, Mabibi na Mabwana.

Itifaki imezingatiwa

Mavazi ya wahitimu yana kofia yenye usinga (tassel). Zamani ni watawa wa ngazi fulani walivaa kofia (mfano maaskofu) kuashiria busara, akili na upeo wa hali ya juu. Vazi hili liliingizwa kwenye mbwembwe za ibada ya mahafali kwa ishara zilezile: busara, akili, na upeo mkubwa. Wahitimu wa shahada ya awali (Bachelors degree) na umahiri (masters degree) kofia zao ni za umbo la sambamba (rhombus). Wahitimu wa shahada ya uzamivu (Doctorate) kofia zao ni umbo la mduara. Usinga kwenye kofia una rangi ya fani aliyosomea muhitimu. Singa zinawekwa upande wa kushoto kwa wahitimu tarajali. Wanapotunukiwa tu shahada, hapo hapo singa wanaziweka upande wa kulia kama ishara kuwa wametoka ngazi moja maishani mwao na kwenda ngazi ya juu.

Hivyo, waliomo humu waliovaa mavazi ya kisomi, wote ambao tayari ni wahitimu wa shahada fulani, singa za kofia waziweke mkono wa kulia. Wahitimu tarajali waziweke mkono wa kushoto; pindi tu wakitunukiwa shahada zao, wazigeuze ziwe mkono wa kulia.

Wapendwa waalikwa:

Kumekuwa na mijadala mingi pindi kiongozi wa nchi anapotunukiwa udaktari wa heshima. Tena kwenye vyombo vya habari ni kawaida kusikia udaktari wa falsafa unachanganywa na udaktari wa heshima. Hivyo si vibaya hadhara iliopo hapa ikapata kueleweshwa aina ya shahada ambazo kwa kawaida chuo kikuu kinaweza kutunuku. Zipo aina nne kama ifuatavyo:

Ndugu Wageni waalikwa:

Awali mavazi ya sherehe za mahafali hayakuwa yamesanifiwa. Mbwembwe za mavazi na nakshi nakshi zake zilianza kusanifiwa karne ya 14 hadi 15 kwenye vyuo vikuu vya Uingereza, baadaye Ulaya kote, na baadaye makoloni ya nchi za ulaya ikiwemo Marekani kaskazini na kusini. Awali majoho (gowns) yenye kifuniko (hood) au vazi la mabegani yalikuwa mavazi ya watawa wa kikristo miaka ya karne ya 5 had ya 15, na wao waliyavaa pia walipokuwa wakifundisha kwevye vyuo vya taasisi zao.

Vyuo vikuu viliyachukulia mavazi haya kuwa mavazi ya kawaida (academic dress) ya wahadhiri na maprofesa. Baadaye mavazi haya yalisanifiwa kuwa mavazi ya mahafali. Kuna mbwembwe nyingi kwenye hayo mavazi, ikiwemo rangi, mistari na maumbo yake kwenye mikono, kitambaa cha ndani ya kifuniko yaani vazi la mabegani na rangi zake, rangi ya joho na kadhalika.

Kwa sasa joho na vazi la begani vinathibitiwa mahsusi na vinaashiria chuo kikuu cha mhitimu, ngazi ipi ya shahada aliyo hitimu, na fani ipi anayotunukiwa mhitimu. Kila fani imepewa rangi yake. Kwa sasa Chuo kikuu chetu kina toa wahitimu kwenye skuli kuu tatu na kila skuli ina rangi yake kama ifuatavyo:

- **Rangi ya kijani**: Skuli kuu ya Sayansi ya Uhai na Uhandisi Baiolojia;
- **Rangi ya samawati**: Skuli kuu ya Rasilimali vitu, Nishati, Maji na Sayansi ya Mazingira; na
- **Rangi nyekundu**: Skuli kuu ya Sayansi na Uhandisi wa Ukokotoaji na Mawasiliano

Mheshimiwa Mkuu wa Taasisi na wahitimu tarajali mlio tufanya tujumuike hapa leo:

Awali ya yote, mimi Mlau wa sherehe ya mahafali naitwa Profesa Verdiana Grace Masanja, kwa rukhsa ya Mkuu wa Taasisi napenda kuwakaribisha nyote kwenye haya mahafali. **KARIBUNI SANA**.

Mkuu wa Taasisi

Hatuna budi kumshukuru Mwenyezi Mungu Rahim kutuwezesha leo, kushiriki mahafali ya sita ya Chuo Kikuu chetu pendwa, pamoja na changamoto za virusi vya Corona na maradhi ya COVID-19, vinavyoendelea kutikisa ulimwengu mzima. Hakika fadhili zake hazina kifani. Rahim kawaangazia viongozi wa taifa letu, nao wamefanya maamuzi ya kipekee juu ya hili janga, na leo hii tumeweza kuadhimisha mahafali ya sita, huku wenzetu kutoka mataifa mengine mengi hawajui hata lini wataweza kurejea masomoni. Tuzidi kumshukuru kwa neema, rehema, na baraka zake kwa Taifa letu la Jamhuri ya Muungano Tanzania na viongozi wake.

Mheshimiwa mkuu wa taasisi yetu:

Kwa heshima na taadhima naomba umma huu tusimame na kukaa kimya kwa dakika moja kwa heshima ya mpendwa Rais wetu mstaafu, Mh. Benjamin William Mkapa aliyetutoka hivi karibuni. ... **Ahsanteni**

Wapendwa wahitimu, viongozi, na wageni wote mliopo hapa.

Siku ya mahafali ni ibada (ritual) yenye mbwembwe na nakshi vilivyoanza mnamo karne ya 6 au 7 hivi kwa wahitimu wa

madrasat na wanazuoni wa islam din na ikaanza ku rasmishwa kwenye vyuo vikuu karne ya 12. Imekuwa ikisanifiwa tangu miaka zaidi ya 700 na kila mara inasaanisfiwa kufuatana na mazingira na jadi za nchi na taasisi husika.

Mheshimiwa mkuu wa taasisi:

Naomba kwanza niseme kwa ufupi mwanzo wa mahafali, historia fupi ya vionjo vilivyomo kwenye ibada hiyo, yaliyomo katika sherehe za mahafali na alama zake, na nitahitimisha kwa kutaja aina ya shahada ambazo hutunikiwa na vyuo vikuu.

Mheshimiwa mkuu wa taasisi

Dhana ya kupata shahada inatokana na jadi ya kiislam ya kutoa ushuhuda wa maarifa unao mruhusu mtu aliye hitimu mtaala maalumu wa masomo ya Islam dini na madrasa kuthibitishwa kama mtu mwenye maarifa ya mtaala huo na kumruhusu kufundisha wengine maarifa aliyojifunza. Na ilifanyika sherehe ya kutunuku vyeti kwa wahitimu wa mtaala. Inasadikika jadi hii ilianza miaka ya karne 6 au 7, kwa mujibu wa wana historia, mfano Glen Cooper, profesa wa Chuo Kikuu cha Birmingham Young, Uingereza. Tukumbuke kuwa uislam uliingia Afrika kaskazini kwenye karne 6 na Afrika mashariki ukanda wa pwani na visiwani kwenye karne ya 8. Hivyo hata bara letu hususan ukanda wa pwani yetu unao utamaduni huo tangu nyakati hizo. Mfumo wa vyuo vikuu kama vilivyo sasa ulianzishwa kwenye karne ya 12 huko ulaya.

Taifa la Ufaransa lilianzisha mfumo wa maadamano ya wahadhiri na wahitimu kuzunguka mitaa yote ya mji/ jiji husika huku majina ya wahitimu yakisomwa hadharani kusudi wananchi wote wawatambue kuwa hao ni wasomi wahitimu.

Taifa la Uingereza lilianzisha sherehe ya mahafali ambayo ilijumuisha maadamano ya wahadhiri na wanahitimu tarajali na maandamano nayo yalitanguliwa na Mlau. Walikusanyika kwenye uwanja wa taifa. Baada ya maadamano na watu wote kukaa, Mlau alikuwa mtu wa kwanza kusoma hotuba yake. Kisha sherehe nyingine zilifuatia, ambazo ni kuunda mkusanyiko (congregation), kutunuku shahada kwa wahitimu, na kuvunja mkusanyiko.

Mabibi na mabwana:

Maana ya maandamano ni ishara ya kuonyesha furaha kubwa waliyonayo wahadhiri na maprofesa kwa kutoa matunda ya jasho lao la kuwafundisha wanaohitimu siku hiyo. Wote wanavaa mavazi yao rasmi ya kisomi (academic dress). Mlau anabeba rungu (mace) mkono mmoja ambayo ni alama ya mamlaka ya taasisi (na pia mamlaka ya mkuu wa taasisi) inayotunuku shahada. Aidha mkono wa pili Mlau anabeba kitabu ambayo ni alama inayoonyesha kuwa matunda yaliyo zalishwa ni wasomi wenye busara na watakuwa wasomi endelevu (long life learners) watakao tatua changamoto za jamii kupitia maarifa, taaluma, ubunifu na usomi, vinavyopatikana kwenye vitabu.